Miembeni wamtaka Boniface Mkwasa awafundishe

Habari zote na Aboud Mahmoud, Zanzibar

MABINGWA wa soka Zanzibar Miembeni, wana mpango wa kumchukua Charles Boniface Mkwasa ili afundishe timu hiyo baada ya kocha Suleiman Mahmoud Jabir kuhwagi mkwanga.

Habari za uhakika kutoka ndani ya Miembeni zimesema kuwa, tayari mawasiliano baina ya uongozi wa timu hiyo na Mkwasa yamefanyika.

Kiongozi mmoja wa Miembeni ambaye alimba hifadhi ya jina lake, alilizambia Burudani kuwa, mazungumzo yao ya awali yamesikia hatua nzuri na wana uhakika wa kumpata kocha huyo.

Alisema wakati wakiendelea na mazungumzo, timu yao kwa sasa itakuwa chini ya Saidi Kaimbi aki saidiwa na Saleh Machupa. Nahodha atakuwa Ramadhani Kidilu.

Kuondoka kwa Jabir kumekuja siku chache baada ya meneja wa timu hiyo Hashim Selemi kutangulia kuachia wadhifa wake.

Mwaka jana aliekuwa kocha wa timu hiyo, Tom Olaba, aliondoka zikiwa zimesalia siku kumi ligi kuu ya Zanzibar kumalizika.

Hiwa chini ya Jabir, Miembeni imetwaa ubingwa wa kombe la Mapinduzi.

Pia alichangana katika mashindano ya klabu bingwa, ambapo Miembeni iliondoshwa robo ya kwanza na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Miembeni wiki hii ilifunga Malindi bao 1-0 katika mechi ya ligi kuu Zanzibar inayoendelea lutimua vumbi.

'Wajukuu wa Makamba' kuwasha moto Z'bar

KUNDI zima la Dar es Salaam Modern Taarab 'Wajukuu wa Makamba', wanatarajia kufanya maonyesho ya muziki Zanzibar.

Kundi hilo limalotamba kwa sasa katika anga za muziko uipisho, litaanza kutumbuiza kesho kwenye ukumbi wa Gymkana.

Akizungumza na gazeti hili juzi, meneja wa kituo cha Burudani cha redio Bondeo FM Talib Suleiman alisema, onesho hilo ni moja ya mfululizo wa uzinduzi wa kituo hicho kipya cha redio.

Pamoja na uzinduzi wa kituo hicho, kundi hilo pia litafanya uzinduzi wa albamu yao maarufu ya Gharika ya moyo.

Suleiman alisema kuwa, katika onesho hilo kundi la East African Melody litasindikiza.

Aidha, mwigizaji mahiri King Majuto naye atapamba uzinduzi huo unaotarajiwa kuwa ua mvuto.



Mtaalamu wa sanaa na maigizo kutoka Ujerumani Stephanie Gra akizungumza na waatoto mjini Zanzibar juzi. (Picha na Aboud Mahmoud).

Wasanii washauriwa kujiendeleza

WASANII nchini wameshauriwa kujiendeleza kielimu ili kukuza taaluma yao.

Kauli hiyo imetolewa na bendi ya warumuni wa choo cha muziki wa taarab maarufu kama [illegible] ya mahiya maonyesho ya muziki [illegible] Ahmed Fadhili wiki hii.

Wanamuziki hao walisema sio lazima wasomi wasomi wa [illegible] mengine [illegible] wiki [illegible] muziki [illegible] vaidia katika muziki.

Walisema [illegible] wasanii [illegible] kielimu, [illegible] wanawezeshwa kukosa [illegible] wanaoshindwa [illegible].

[illegible] wasanii [illegible] ujuzwa [illegible] chuoni, [illegible] na [illegible] mabadiliko [illegible] Wakati huo [illegible] alisema [illegible] Mwalim Mahmoud.

"Sisi wengine kama [illegible] elimu ya shule lakini tunasaidia tu elimu ya muziki na [illegible] kwa [illegible] kuwa [illegible] chetu," alisema.

Walisema, elimu ya sanaa imekua imbaro [illegible] ya muziki [illegible].

"Wasanii wa Zanzibar [illegible] sana, lakini hatujui [illegible] elimu hii. Wengeni [illegible] wanafunguo [illegible] kwa ajili ya sanaa," alisema Mwalim [illegible].

Chuo cha muziki wa taarab (DCMA) kilichopo Zanzibar, kinatoa [illegible] ya [illegible] muziki [illegible] kwa [illegible].

DCMA yapata mtaalamu

CHUO cha muziki wa nchi za Jahazi (DCMA), kimefanikiwa kumpata mtaalamu wa sanaa ya maigizo na muziki jukwaani.

Mtaalamu huyo kutoka Hamburg, Ujerumani Stephanie Gra, amefika chuoni hapo kwa ajili ya kufundisha walimu wa muziki kupitia sanaa ya maigizo na muziki.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, Afisa Ufusiano wa DCMA Lionie Schollmeyer, alisema mwalimu huyo atasaidiana na mwalimu mmoja wa chuo hicho.

Alimtaja mwalimu huyo kuwa ni Said Vuwai ambae kwa hivi sasa tayari wameshaandaa igizo la Jumping Mouse.

Alisema, pia wameandaa igizo jingine litakalofahamisha kama Sisimzi.

Alisema, katika maigizo hayo wameweshirikisha wanafunzi wa shule za msingi.

Alizitaja shule zinashirikiana na mtaalamu huyo kuwa ni shule ya Smile Future, Tanzania Global Academy na Living Stone.

Mtaalamu huyo atakapomaliza muda wake, Vuai ndiye atawendeleza kutoa elimu hiyo kwa walimu wengine.